

## Maendeleo ya Awali ya Mtoto **Utoto wa kati**

Watoto kati ya miaka 5-11, wanahitaji watu ambao ni mifano bora katika maisha yao. Wanaona pale ambapo watu wazima hawafanyi kile wanachokisema.

Unaweza kuwa mfano bora kwa watoto wako kwa:



1. Kujijali na kujiweka katika hali nzuri wewe binafsi.
2. Kuwa makini na maneno na matendo yako. Unapaswa kuyaishi yale unayomwelekeza mtoto wako.
3. Kuomba msamaha pale unapokuwa umekosea. Usitafute sababu za kujitetea.
4. Kuwasikiliza watoto bila kuwahukumu na kujenga uhusiano mzuri nao.
5. Kuwaelekeza kuwa na tabia njema na kuwapongeza wanapofanya vizuri badala ya kuwaadhibu.